Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

MWONGOZO WA KUANDAA NA KUTEKELEZA MIPANGO YA MAENDELEO YA KILIMO YA WILAYA

Decemba 2009

Dar es salaam

YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI.....3
2.0 MCHAKATO WA KUANDAA MIPANGO YA MAENDELEO YA KILIMO NA MIFUGO YA WILAYA.....3
2.1 Uchaguzi na Upangaji wa Vijiji kwa Awamu (Village phasing in/out plan) 3
2.2 Uandaaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo na Mifugo ya Wilaya.....3
2.2.1 Ngazi ya Kijiji.....4
2.2.2 Ngazi ya Kata.....5
2.2.3 Ngazi ya Wilaya.....4
2.2.4 Ngazi ya Mkoa.....4
2.2.5 Ngazi ya Taifa.....5
3.0 UANDAAJI WA ANDIKO LA MIRADI YA UWEKEZAJI.....6
3.1 UMUHIMU WA KUFANYA MCHANGANUO WA GHARAMA NA MANUFAA YA MRADI (COST AND BENEFIT ANALYSIS).....6
4.0 UGHARAMIAJI WA DADPs.....6
4.1 Matumizi ya ruzuku.....7
5.0 KUHAKIKI MIRADI (PROJECT APPRAISAL).....9
6.0 UPATIKANAJI NA USIMAMIZI WA FEDHA.....9
7.0 MANUNUZI NGAZI YA KIJIJI.....10
8.0 MASUALA MTAMBUKA: UHIFADHI WA MAZINGIRA, JINSIA, VVU/UKIMWI, USALAMA WA CHAKULA, MASOKO, MATUMIZI YA ARDHI NA UPASHANAJI HABARI.....11
8.1 MAZINGIRA.....11
8.2 JINSIA , VVU/ UKIMWI.....12
8.3 USALAMA WA CHAKULA.....13
8.4 MASOKO.....13
8.5 MATUMIZI BORA YA ARDHI.....13
8.6 UPASHANAJI HABARI.....14
9.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI YA DADPs.....14

VIAMBATISHO.....16
Kiambatisho Na.1: Hatua za kuzingatia katika uandaaji wa andiko la mradi...16
Kiambatisho Na. 2: Bao Mantiki (Logical Framework).....18
Kiambatisho Na.3: Utaratibu wa uchangiaji katika kutekeleza miradi mbalimbali ya uwekezaji katika jamii/vikundi.....20
Kiambatisho Na. 4: Vigezo vinavyotumika kuhakiki mradi.....20
Kiambatisho Na 5: Jinsi ya kuchanganua Gharama na Manufaa (Cost-Benefit Analysis) ya Mradi.....21
Kiambatisho Na 6: DADP STRUCTURE.....25

1.0 UTANGULIZI

Mwongozo huu utatumika katika halmashauri zote za Serikali za mitaa katika kupanga, kutekeleza, kusimamia, kufuatilia na kutathmini Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(District Agricultural Development Plans* – DADPs) kwa kuzingatia vipaumbele vilivyopitishwa na mkutano mkuu wa jamii husika kupitia mchakato wa Mbinu Shirikishi Jamii ya Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo *(Opportunities and Obstacles to Development - O & OD).* Lengo la mwongozo huu ni kutoa maelekezo kwa watendaji wa ngazi mbalimbali jinsi ya kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo *(Agricultural Sector Development Programme - ASDP)* ambayo katika ngazi ya Wilaya hutekelezwa kupitia DADPs.

2.0 MCHAKATO WA KUANDAA MIPANGO YA MAENDELEO YA KILIMO NA MIFUGO YA WILAYA

Mchakato huu utahusisha uchaguzi wa vijiji vya kutekeleza DADPs kwa awamu, uibuaji na uandaaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Vijiji (*Village Agricultural Development Plans-VADPs*) ambayo hujumuishwa na kuwa DADPs.

2.1 Uchaguzi na Upangaji wa Vijiji kwa Awamu (Village phasing in/out plan*)*

Ili kuwa na miradi yenye kuleta tija halmashauri ni lazima ichague **idadi** ya vijiji kulingana na **vipaumbele** vya halmashauri pamoja na **kiasi cha ruzuku** ya uwekezaji iliyotengwa kwa halmashauri. Vigezo muhimu vya kuzingatia wakati wa kuchagua vijiji ni pamoja na: kuwepo kwa fursa za kilimo, utayari wa jamii na uongozi wa kijiji kushiriki kwenye shughuli za kilimo na mifugo kwa kuchangia na kufanya kazi, kuwepo kwa miradi ya kilimo inayoendelea na kuwepo na fursa za masoko. Kila kijiji kilichochaguliwa kwenye awamu ya utekelezaji kitatengewa ruzuku za maendeleo ya kilimo kiasi kisichopungua shilingi milioni 56 kwa ajili utekelezaji wa miradi ya uwekezaji. Kiwango hicho cha fedha ndicho kitakachoelekeza idadi ya vijiji vya utekelezaji.

2.2 Uandaaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo na Mifugo ya Wilaya

Mchakato wa kuandaa DADPs utafuata hatua zote kama zilivyoainishwa katika Mbinu Shirikishi Jamii ya Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo *(Opportunities and Obstacles to Development - O & OD).* Timu za wawezeshaji wa kata (*Ward Facilitation Teams*-WFTs) na Wilaya (*District Facilitation Teams*- DFTs) zitasimamia mchakato wote hadi Mipango ya Maendeleo ya Kilimo na Mifugo ya Vijiji *(Village Agricultural Development Plans - VADPs)* itakapokamilika, kupitishwa katika ngazi zote za uongozi na kuwasilishwa Wilayani.

2.2.1 Ngazi ya Kijiji

Katika ngazi ya kijiji mchakato wa kuibua fursa na vikwazo vya maendeleo utafanyika kwa pamoja kati ya wanakijiji na Wawezeshaji wa Kata chini ya uongozi wa Mtendaji wa Kata kwa kufuata taratibu zote za O&OD. Kwa kuwa zoezi la O & OD halifanyiki kila mwaka inabidi Halmashauri ihakiki vipaumbele vya jamii kwa kufanya ***Extended O&OD*** wakati wa kuandaa *na* kuhuisha mipango ya kilimo na ufugaji ya vijiji ya kila mwaka. Extended O&D iangalie zaidi vipaumblele vya kilimo na mifugo. Wawezeshaji ngazi ya kata na wilaya watashirikiana na wakulima kubaini na kuweka vipaumbele kwa **kutumia mbinu** shirikishi na zana zake kama **vile mti wa matumaini** na **mti wa matatizo**.

Uundaji wa kamati ya kusimamia Miradi
Kila kijiji kinachotekeleza DADPs kitachagua kamati za usimamizi wa miradi kwa miradi ya jamii na ya vikundi.
Miradi ya Jamii: Mkutano Mkuu wa kijiji utateua kamati ya watu wenye sifa stahili wasiozidi kumi (10) na wasiopungua wanane ambao watasimamia utekelezaji wa ***mradi wa jamii.*** Wanakamati watachagua viongozi wa kamati ambao ni Mwenyekiti,Makamu Mwenyekiti, Katibu na Mhazini. Wajumbe wawili (2) watachaguliwa kuungana na viongozi wawili wa kamati ya mradi kwa ajili ya kutia saini kwenye nyaraka za fedha, ikiwa ni pamoja na kutoa fedha benki. Inapendekezwa wanawake wasipungue asilimia 50 kwenye kamati ya usimamizi ya mradi pamoja na mwanamke mmoja katika watia saini.

Miradi ya vikundi: Kwa upande wa miradi ya vikundi kazi ya mkutano mkuu itakuwa kupendekeza majina ya vikundi ambavyo vitapata miradi. Wanavikundi watakaa na kuchagua viongozi na kamati ya utekelezaji kwa kuzingatia mchanganyiko wa kijinsia kama ilivyo kwenye mradi wa jamii. Inapendekezwa vikundi viwe na wanachama wasiopungua 20 na wasiozidi 40 kutoka kaya tofauti.

Angalizo: *Vikundi viwe vimeundwa kwa kuzingatia misingi ya kuunda vikundi ili kuwa uendelevu.* ***Idadi ya wajumbe*** *wa Kamati ya mradi wa kikundi itategemea idadi ya wanakikundi, lakini wasizidi 10 na wasipungue watano.*

Kamati za miradi ya jamii na vikundi zitawajibika kwa uongozi wa serikali ya kijiji kutoa taarifa za mara kwa mara za maendeleo ya miradi yao ikiwa ni pamoja na taarifa za mapato na matumizi ya fedha. Aidha kamati hizi hazitaruhusiwa kutoa fedha kwenye akaunti zao bila kuwa na muhtasari ambao utaridhiwa na kusainiwa na viongozi wa serikali ya kijiji na zilizopitishwa na kuidhinishwa na halmashauri ya wilaya. Mtendaji wa kijiji atagonga muhuri baada ya kutia saini yake au ya Mwenyekiti ili kudhibiti matumizi ya fedha za umma.

- **Kazi za kamati za miradi**

Kazi za kamati ni pamoja na: (i) Kupanga na kuandaa andiko la mradi; (ii) Kuhamasisha na kukusanya michango mbalimbali ya wanajamii au wanakikundi kulingana na aina ya mradi kama mwongozo unavyoelekeza; (iii) Kuandaa mpango kazi; (iv) Kusimamia mchakato wa utekelezaji; (v) Kusimamia matumizi ya fedha za mradi na ununuzi wa bidhaa na huduma; (vi) Kutafuta vyanzo mbalimbali vya huduma na teknolojia; (vii) Kusimamia na kulinda mali zote za mradi; na (viii) Kutoa taarifa za utekelezaji pamoja na mapato na matumizi ya fedha na kuwasilisha kwa wanakikundi na serikali ya kijiji.

2.2.2 Ngazi ya Kata

Wawezeshaji wa Kata chini ya uongozi wa Mtendaji wa Kata wanapaswa kupitia na kuunganisha mipango ya vijiji pia kubaini na kuratibu utekelezaji wa miradi itakayohusisha zaidi ya kijiji kimoja.

2.2.3 Ngazi ya Wilaya

Utekelezaji wa DADPs ngazi ya wilaya utasimamiwa na Afisa Kilimo na Mifugo wa Wilaya. Wawezeshaji wa Wilaya chini ya uongozi wa Afisa Mipango wa Wilaya wanapaswa kuhuisha/kujumuisha mipango ya maendeleo ya kilimo ya vijiji vilivyochaguliwa ili kuunda Mpango wa Maendeleo wa Kilimo wa Wilaya.

2.2.4 Ngazi ya Mkoa

Katika ngazi ya mkoa kutakuwa na Mratibu wa ASDP ambaye ataratibu utekelezaji wa DADPs katika mkoa wake kulingana na Hadidu za Rejea alizopatiwa. Atapaswa kusimamia mchakato mzima wa upangaji na utekelezaji wa DADPs katika halmashauri zote kwa kuzingatia mwongozo uliotolewa hususan suala zima la uchaguzi wa vijiji, upelekaji na usimamizi wa fedha katika Halmashauri na vijiji, uandaaji wa maandiko ya miradi, uandaaji wa taarifa za utekelezaji n.k

2.2.5 Ngazi ya Taifa

Katika ngazi ya Taifa kutakuwa na Timu ya Wawezeshaji ambayo imepewa majukumu ya kusimamia uandaaji na utekelezaji wa DADPs katika mikoa yote kulingana na muongozo uliotolewa.

3.0 UANDAAJI WA ANDIKO LA MIRADI YA UWEKEZAJI

Mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kutayarisha andiko la mradi ni kama ifuatavyo:

- Mradi uwe katika mpango wa maendeleo ya kilimo wa kijiji kilichoingia kwenye awamu ya utekelezaji wa DADPs kwa mwaka husika. Fuata hatua za uandaaji wa andiko la mradi kama ilivyoelekezwa kwenye *Kiambatisho Na.1*
- *Andaa bao mantiki la mradi husika.* kama ilivyoelekezwa kwenye *Kiambatisho Na.2*
- Fanya mchanganuo wa gharama na manufaa (*cost-benefit analysis*) ya mradi.

3.1 UMUHIMU WA KUFANYA MCHANGANUO WA GHARAMA NA MANUFAA YA MRADI (COST AND BENEFIT ANALYSIS)

Ni mchakato wa kuchanganua gharama za mradi zikilinganishwa na manufaa yake. Mradi wenye tija ni ule ambao manufaa yake yanazidi gharama za uwekezaji na uendeshaji na yanaweza kuwa ya kifedha, kiuchumi na ya kijamii. Mchanganuo au upembuzi wa gharama na manufaa unapofanywa kwa makini husaidia yafuatayo;

a) Kufanya maamuzi kuhusu matumizi bora ya rasilimali haba kwa manufaa ya jamii.
b) Kubaini maeneo/vipengele vya kupitia ili kuboresha gharama za uwekezaji.
c) Kubaini faida ya mradi kwa mtazamo wa walengwa

Hatua za upembuzi wa gharama (cost benefit analyses) umefafanuliwa kwenye *kiambatisho Na.5*

4.0 UGHARAMIAJI WA DADPs

DADPs zitatekelezwa kwa kutumia ruzuku za maendeleo ya kilimo ambazo zimegawanyika katika makundi matatu kama ifuatavyo ;

(i) Ruzuku ya Uwekezaji *(District Agricultural Development Grant-DADG)*,
(ii) Ruzuku ya Ugani (*Agricultural Extension Block Grant - AEBG),*
(iii) Ruzuku ya Kujenga uwezo *(Agricultural Capacity Building Grant–ACBG).*

Ruzuku hizo zimegawanyika katika makundi mawili, ruzuku ya msingi na ya nyongeza.

Ili Halmashauri ya wilaya iweze kupata ruzuku za nyongeza (DADG, AEBG na ACBG) inapaswa itimize masharti ya msingi ya kupata Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGCDG) na pia itimize masharti yaliyowekwa na Wizara za Sekta ya Kilimo. Sehemu ya Msingi ya Ruzuku itatolewa bila ushindani bali kwa

kufuata fomula. Ruzuku ya nyongeza itatolewa baada ya kufuzu vigezo vitakavyokuwa vimewekwa na sekta ya kilimo ma mifugo.

Aidha, wilaya zitakuwa na fursa za kuomba fedha za nyongeza kutoka kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji wa Wilaya (*District Irrigation Development Fund-DIDF*) ili kutekeleza mipango ya umwagiliaji katika halmashauri kwa miradi ya ukubwa wa kati ambayo gharama zake hazitazidi shilingi milioni mia tano (500,000,000). Mfuko huu ni wa ushindani ambapo halmashauri husika zitaandika michanganuo ya miradi ya aina hiyo na kushindanishwa katika ngazi ya taifa ili kupata miradi yenye ubora wa kufadhiliwa. Vigezo ambavyo vitazingatiwa ni kama ifuatavyo;

i. Halmashauri ziwe tayari kuchangia mradi ya umwagiliaji
ii. Wanufaikaji wanatakiwa kuchangia nguvu kazi au fedha katika ujenzi wa skimu.

Kadhalika, Halmashauri zinatakiwa kutumia **vyanzo vingine** vya fedha zikiwemo Ruzuku ya Maendeleo ya Wilaya (LGCDG), Mapato ya Halmashauri, Taasisi zisizo za Kiserikali na Miradi inayoendelea. Aidha, vyanzo vyote vya fedha lazima vionyeshwe wakat wa kuandaa MTEF.
Michango ya jamii/vikundi ni lazima ikamilishwe kabla ya fedha za miradi husika kutumwa katika akaunti za miradi. Jamii itachangia fedha taslimu, vifaa na nguvu kazi kulingana na aina ya miradi. Utaratibu wa uchangiaji ni kama inavyoonyesha katika *Kiambatisho Na. 3.*

4.1 Matumizi ya ruzuku

(i) Ruzuku ya Uwekezaji

Ruzuku hii ni mahsusi kwa ajili ya kutekeleza miradi iliyoibuliwa na jamii na ni sharti ipelekwe kwenye akaunti za miradi husika mara baada ya kupitishwa na Baraza la Madiwani. Kijiji kilichochaguliwa kitatengewa ruzuku ya uwekezaji kiasi kisichopungua **shilingi milioni 56**. Kati ya fedha hizo **shilingi milioni 40** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya uwekezaji ya jamii isiyozidi 2 na shilingi milioni 16 kwa ajili ya miradi ya vikundi isiyozidi 4. Fedha hizi zote zitapelekwa kijijini moja kwa moja. Matumizi ya ruzuku ya msingi (basic) na nyongeza (top-up) kwa ajili ya kugharamia uwekezaji na maendeleo ya kilimo na mifugo ni kama ifuatavyo;

- **Ujenzi/ukarabati wa miundombinu kama vile:**
  Barabara za vijijini, malambo, majosho, masoko, miradi ya umwagiliaji, machinjio, minada, mabucha, visima na maghala.
- **Uwekezaji katika kuendeleza teknolojia kama vile:**

Ununuzi wa matrekta makubwa na madogo, mashine za kusindika mazao, zana za kukokotwa na wanyama kazi, matumizi ya mifugo bora, matumizi ya mbegu na miche bora

- **Miradi ya hifadhi ya Mazingira kama vile:**
  Kuziba makorongo (gulls) yaliyotokana na mmonyoko wa udongo, kupanda miti n.k.

> **Angalizo:** *Fedha za nyongeza za DIDF zitakazopelekwa katika halmashauri kutekeleza miradi ya umwagiliaji iliyoibuliwa katika vijiji vilivyochaguliwa zinapaswa kupelekwa katika akaunti za miradi husika kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo.*

(ii) Ruzuku ya Kujenga Uwezo:

Ruzuku hii imegawanyika katika sehemu mbili kuu ambazo ni ;

(i) **Ruzuku ya Msingi ambayo** itagharamia mafunzo ya muda mfupi na kujenga uwezo wa halmashauri katika kuandaa na kusimamia utekelezaji wa DADPs na kununulia vitendea kazi (komputa, photocopy, gari, pikipiki, samani za ofisi)

ii) **Ruzuku ya Nyongeza** ambayo itagharamia kujenga uwezo kwa kamati za usimamizi wa miradi, wakulima na watoa huduma kutoka sekta binafsi kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali yanayoendana na miradi waliyoibua (*taylor made demand-driven training*) kama vile manunuzi, utunzaji fedha na kumbukumbu, ujasiriamali, uundaji na uimarishaji vikundi, mafunzo ya usimamizi wa mkataba ya watoa huduma binafsi, mitandao ya wakulima na kufanya ziara za kimafunzo.

Kila kijiji kilichochaguliwa kitapewa ruzuku ya kuwajengea uwezo kisichopungua shilingi **5, 600,000** ambazo ni sawa na asilimia 10 ya ruzuku ya uwekezaji kwa miradi ya jamii na vikundi. Fedha hizi zitatumika katika kutoa mafunzo mahsusi kwa miradi ya vikundi/jamii kama ifuatavyo: *Kujenga uwezo kwa kamati za usimamizi wa miradi kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali yanayoendana na miradi waliyoibua (taylor made demand-driven training) kama vile manunuzi, utunzaji fedha na kumbukumbu, ujasiriamali, uundaji na uimarishaji vikundi, usimamizi wa mkataba ya watoa huduma binafsi, mitandao ya wakulima na kufanya ziara za mafunzo.*

(iii) Ruzuku ya Huduma za Ugani:

Ruzuku hii imegawanyika katika sehemu kuu mbili ambazo ni ;

i) **Ruzuku ya Msingi** ambayo itagharamia uendeshaji wa huduma za ugani kama vile, utoaji wa chanjo, utafiti, uwezeshaji wa wataalam, ununuzi wa vitendea kazi (extension kits, shajala)

ii) **Ruzuku ya nyongeza** ambayo itagharamia ujenzi wa vituo vya kilimo vya taaluma vya kata (*ward agricultural resource centres*), mikataba kati ya halmashauri na watoa huduma, mikataba kati ya watoa huduma na wakulima, kuunda na kuimarisha vikundi na mitandao ya wakulima,mafunzo kwa mitandao ya wakulima na kushiriki katika maonesho (Nane Nane, *Farmer Field Days n.k*).

Kila kijiji kilichochaguliwa kitapewa ruzuku ya huduma za ugani kiasi kisichopungua shilingi **5,600,000** ambazo ni sawa na asilimia 10 ya ruzuku ya uwekezaji. Ruzuku hii ya huduma za ugani itatumika kama ifuatavyo: *Mikataba kati ya watoa huduma na wakulima, kuunda na kuimarisha vikundi na mitandao ya wakulima, mafunzo kwa mitandao ya wakulima na kushiriki katika maonesho (Nane Nane, Farmer Field Days n.k).*

Angalizo:

1. Ruzuku ya Kujenga uwezo (CBG) *haitagharamia* mafunzo au kozi za muda mrefu kama vile shahada ya kwanza na ya pili (BSc and MSc). Aidha ruzuku itaendelea kugharamia masomo ya wanafunzi ambao tayari wako masomoni.
2. Halmashauri ambazo hazitapanga mipango yake kwa kuzingatia uchaguzi wa vijiji na kuonyesha matumizi ya fedha za ruzuku zilizotajwa kama muongozo unavyoonyesha hazitapelekewa fedha.
3. Fedha za ruzuku zitumike jinsi zilivyoidhinishwa na Bunge la bajeti.

5.0 KUHAKIKI MIRADI (PROJECT APPRAISAL)

Ili kuweza kuhakiki iwapo andiko la mradi limeandikwa inavyostahili ni muhimu kufanya uhakiki wa miradi ofisini (*Desk appraisal*) na kwenye eneo la mradi (Field Appraisal). Uhakiki hufanywa na timu ya wawezeshaji wa wilaya (DFT) chini ya usimamizi wa DALDO na DPLO katika ngazi ya Wilaya na RS na NFT katika ngazi ya Taifa. Mambo muhimu ya kuzingatia ni pamoja na: (i) Kuangalia kama andiko linaendana na malengo na majukumu ya ASDP (ii) Kuwepo kwa mradi kwenye orodha ya vijiji vilivyoingia kwenye awamu ya utekelezaji wa DADP; (iii) Athari za mradi kwa mazingira; na (iv) Mchanganuo wa gharama na manufaa. Vigezo vinavyotumika kuhakiki mradi ni kama inavyoonekana kwenye *Kiambatisho Na.4.*

6.0 UPATIKANAJI NA USIMAMIZI WA FEDHA

Wizara ya Fedha na Uchumi itatuma fedha za utekelezaji wa DADPs kwenye akaunti ya maendeleo ya Halmashauri. Kila kijiji au kikundi chenye mradi kinapaswa kufungua akaunti yake itakayoendeshwa na kamati ya mradi husika. Mkurugenzi Mtendaji atahamisha pesa za kila mradi kwenda kwenye akaunti ya

mradi kwa utekelezaji baada ya wanufaika kufungua akaunti na kuchangia gharama za mradi wanazotakiwa kuchangia. Taratibu za matumizi ya fedha zitafuata mfumo wa Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa (LGCDG). Wakurugenzi wote watahakikisha kuwa:-

- Halmashauri inaandaa ripoti ya fedha na kujadiliwa na menejimenti
- Ripoti za fedha kutoka kwenye miradi ya jamii/vikundi au wakulima zinaandaliwa na kuwasilishwa kwenye ofisi ya Mkurugenzi kwa ajili ya majumuisho.
- Kuhakikisha kuwa ripoti zinaonyesha bayana aina ya fedha na matumizi yake sahihi. Kama vile DADG, CBG, EBG na DIDF zikionyesha bajeti, jinsi zilivyoingia na matumizi yake.
- Kuonyesha fedha zilizobakia na matumizi yake kwenye mwaka mwingine wa fedha (Roll over funds). Halmashauri zote ambazo zitakuwa na fedha ambayo haijatumika (carry over fund) kiasi hicho kitazingatiwa katika mgao wa bajeti ya mwaka unaofuata.

7.0 MANUNUZI NGAZI YA KIJIJI

Ununuzi wa bidhaa zote na huduma katika ngazi ya jamii ufanywe na kamati ya Mradi kwa kufuata ushauri wa wawezeshaji wa kata na wilaya kwa kuzingatia sheria na kanuni za manunuzi zilizopo. Kamati za miradi sharti zipatiwe mafunzo na DFT kuhusu kanuni za manunuzi na taratibu za matumizi ya fedha na utunzaji wa kumbukumbu.

Manunuzi yote yatatangazwa kwenye mbao za matangazo ili kuwajulisha wanakijiji na watoa huduma na kutoa ushindani katika manunuzi. Manunuzi yatafanyike katika taratibu zifuatazo:

i) **Manunuzi ya kawaida (Local shopping)**: Utaratibu huu unafanyika kwa kutumia dondoo (Quotations). Kiasi cha dondoo tatu kitatumiwa kwa kila *order* ya huduma na bidhaa.

ii) **Manunuzi kwa kutumia zabuni za kawaida (Local Bidding)**: Hii ni sawa na zabuni za ushindani katika ngazi ya taifa (National Competitive Bidding) ila inarahisishwa kwa ajili ya ngazi ya wilaya na mkoa. Hii inatumika kwa ajili ya mikataba mikubwa. Matangazo ya zabuni za aina hii yanahitaji tangazo maalum ambalo litawekwa kwenye maeneo ya mikusanyiko ya watu yaliyopo kijijini, wilayani na mkoani.Vilevile itatumia njia za asili kutangaza. Zabuni hii itatumia muda wa siku kumi na tano mahala na muda wa ufunguzi utatakiwa kuonyeshwa.

iii) **Manunuzi ya kutumia mikataba (Direct Contracting/Source)**: Hii itatumika pale itakapoonekana kuwa utumiaji wa njia nyingine utaongeza gharama bila sababu ukilinganisha na njia hii.Vilevile pale ambapo kuna mtoa huduma mmoja tu katika eneo husika.

iv) **Akaunti ya pamoja ya jamii (Community Force Account)**: Njia hii hutumika pale ambapo jamii itatekeleza miradi midogomidogo kwa

kutumia rasilimali yake yenyewe (skilled and unskilled labour, materials, equipment) kama sehemu ya mradi.

v) **Wataalam waelekezi (Consultants**): Hawa wanaweza kuwa; Mtaalam Binafsi (Individual Consultant) au Kampuni (Firm). Wataalam hawa watachaguliwa kutokana na ujuzi/utaalam katika kazi husika kwa kuwashindanisha wale watakao kuwa tayari kushiriki. Orodha ya wataalam hao itatayarishwa na kuhifadhiwa na pale watakapo hitajika watashirikishwa kufanya hivyo.

vi) **Uhakiki wa awali (Prior Review of threshold)**: Hakuna huhakiki wa awali ambao hutahitajika (prior review)

vii) **Udhibiti wa manunuzi (Peer Control)**: Wafadhiliwa (beneficiaries) watawakilishwa/watashirikishwa moja kwa moja katika kudhibiti pesa walizopangiwa.

8.0 MASUALA MTAMBUKA: UHIFADHI WA MAZINGIRA, JINSIA, VVU/UKIMWI, USALAMA WA CHAKULA, MASOKO, MATUMIZI YA ARDHI NA UPASHANAJI HABARI

Masuala yote yanayohusu mazingira, jinsia, VVU/UKIMWI, usalama wa chakula, masoko, matumizi ya ardhi na upashanaji habari yanapaswa kuzingatiwa wakati wa kuibua, kupanga, kutekeleza, kufuatilia na kutathmini mradi.

8.1 MAZINGIRA

Masuala ya mazingira yazingatie mwongozo wa Mazingira wa Miradi ya ASDP (*Environment and Social Managenent Framework* -ESMF), kwa muhtasari kama ifuatavyo:

Aina za Miradi inayohitaji tathimini ya Athari ya Maazingira (EIA)

Hatua ya kwanza ili kufanyika *Environmental Impact Assessment (EIA)* katika miradi inayofadhiliwa na ASDP ni kufanya "Screening" kwa njia ya PRA. Hatua ya kufanya PRA utatoa makundi ya miradi kulingana na ukubwa wake. Kulingana na ESMF ya ASDP miradi ya kundi A ni ile mikubwa ambayo kulingana na gharama zake haitafadhiliwa na ASDP na hii lazima ifanyiwe EIA kabla ya kuanza utekelezaji wake. Miradi ya kundi B na C inaweza kufadhiliwa na ASDP. Miradi ya kundi B kutokana na (i) aina, (ii) ukubwa na (iii) utekechu (sensitiveness) wa eneo utakapotekelezwa inaweza ikalazimu kufanyika au kutofanyika EIA. Miradi ya kundi C ambayo asilimia kubwa ndiyo inayotekelezwa na jamii na vikundi chini ya DADPs itafanyiwa "Screening". Utaratibu wa kufanya "Screening" huanza mara moja mradi unapoibuliwa.

Mambo ya kuzingatia wakati wa kufanya "Screening" ni kama yafuatayo:

- Je mradi utachangia uharibifu wa mali asili?

- Je mradi utasababisha uchafuzi wa ardhi, maji au hewa?
- Je mradi utasababisha/ utachangia kuhamisha watu au jamii ya watu?
- Je mradi utasababisha madhara kwa afya?
- Je mradi utasababisha/ utachangia mabadiliko ya Sera mfano: Sera ya maji?
- Je mradi utaathiri maisha ya watu au jamii inayoishi katika eneo husika kwa kuongeza matumizi ya maliasili zilizopo?
- Je mradi utasababisha migogoro juu ya hati miliki ya eneo utakapotekelezwa au mabadiliko ya hati miliki ya eneo la mradi?
- Je mradi utasababisha migogoro juu ya athari zinazoweza kutokea baadaye katika mazingira?
- Kuhakikisha mradi hautachangia uharibifu wa ardhi na mmomonyoko wa udongo. Tuepuke miradi ya kilimo kisichozingatia hifadhi ya udongo au kufuga mifugo kushinda uwezo wa malisho, kutofyeka misitu, mradi au shughuli zake zisiwe katika au karibu na maeneo yenye vyanzo vya maji, kando kando ya mito, maziwa, mabwawa na maeneo oevu,
- Kutokuwa na shughuli za ujenzi au kuchimba mchanga, udongo, mawe kando ya mito, maziwa, mabwawa na maeneo oevu au kwenye maeneo yenye kumbukumbu muhimu za kihistoria au kijamii
- Eneo la mradi lizingatie mipango ya matumizi bora ya ardhi kama ilivyokubalika na kijiji (Kuhakikisha miradi haitachangia upotevu wa bioanuai na uoto wa asili ili kutoathiri mfumo wa maisha (Ecosystem) wa eneo husika,
- Kuhakikisha miradi haitachangia mabadiliko ya tabianchi mfano upotevu wa misitu na yale yaliyotajwa katika (i) hapo juu,
- Kudhibiti uchafuzi wa mazingira utakaosababishwa na kuwepo kwa mradi mfano; namna ya kushughulikia tatizo la takataka zitakazotokana na kuwepo kwa mradi kama wa soko.
- Kuwa na matumizi sahihi ya viuatilifu katika kudhibiti visumbufu, mfano; shughuli za uzalishaji mboga na matunda, majosho ya kuogeshea wanyama. (Mambo ya kuzingatia: Nunua viuatilifu sahihi, kiasi na muda sahihi wa kununua na kutumia, usafirishaji na uhifadhi wake, mavazi yanayotakiwa wakati wa kutumia, kuzingatia maelezo ya matumizi, usafi wa vyombo vilivyotumika na udhibiti wa vyombo na viuatilifu vilivyokwishatumika.

8.2. JINSIA , VVU/ UKIMWI

Mwongozo unasisitiza kwamba;

i) miradi izingatie maslahi ya makundi mbalimbali kuhusiana na jinsia zao mathalani vijana, wazee, wanawake, watoto na wanaume.

ii) takwimu za utekelezaji wa miradi zioneshe idadi ya watu walionufaika kulingana na jinsia zao,

iii) kuwe na miradi inayolenga kutekeleza mahitaji ya makundi maalumu kama waarithika wa VVU/UKIMWI
iv) takwimu zitakazokusanywa zioneshe idadi ya watu wa makundi maalum ya walionufaika na miradi ya DADPs.

8.3 USALAMA WA CHAKULA

Wakati wa kuibua, kupanga, kutekeleza na kutathmini miradi ya kijiji ni muhimu jamii ishirikishwe:

Kutambua makundi yaliyo katika hali hatarishi (vulnerables) hususan, walemavu, wajane na wagane, kaya zinazoongozwa na watoto na wazee, kaya zinazokabiliwa na matatizo ya usalama wa chakula, wenye upungufu mkubwa wa ardhi na rasilimali nyingine n.k.

Makundi yawezeshwe kupanga, kutekeleza na kutathmini miradi ya kutatua matatizo ya usalama wa chakula na uhakika wa kipato ili yajihakikishie usalama wa chakula, kujiongezea kipato na yaweze kushiriki na kuchangia katika shughuli za maendeleo.

8.4 MASOKO

Masuala yote yanayohusu masoko yanapaswa kuzingatiwa wakati wa kuibua, kupanga, kutekeleza na kutathmini miradi ya kilimo na mifugo kama ifuatavyo:

i. Kuhahikisha miradi inawawezesha wakulima kuzalisha mazao ambayo yanakidhi mahitaji ya soko kwa kuzingatia ubora, kiasi na ufungashaji.
ii. Kuhakikisha ununuzi wa mazao unazingatia upangaji wa madaraja na matumizi sahihi ya vipimo.
iii. Kushirikiana na Sekta Binafsi kuhakikisha wakulima wanapata taarifa muhimu za masoko ya mazao ya Kilimo na Mifugo ndani na nje ya nchi.
iv. Kushirikiana na Sekta Binafsi kuhamasisha wakulima kuunda vikundi ambavyo vitasaidia wakulima kuwa na nguvu katika mfumo wa soko huru ikiwa ni pamoja na uanzishaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani na Kilimo cha Mkataba
v. Kuhakikisha wakulima wanahamasishwa na kupata elimu kuhusu usindikaji na uongezaji thamani katika mazao ili kuondokana na upotevu wa mazao baada ya kuvuna.

8.5 MATUMIZI BORA YA ARDHI

i) Kijiji kipange matumizi bora ya ardhi, ambapo maeneo ya kilimo na mifugo yataweza kupangiwa usimamizi wa matumizi endelevu.
ii) Kutekeleza teknolojia sahihi za matumizi bora ya ardhi zitakazoongeza tija ya ardhi ya kilimo na mifugo kama uzuiaji wa mmomonyoko wa udongo, utumiaji wa mbolea na kwa kiwango sahihi.

iii) Kuhakikisha kuwa hakuna migogoro inayohusu matumizi ya ardhi kati ya makundi mabalimbali kijijini

8.6 UPASHANAJI HABARI

(i) Halmashauri ziwajengee uwezo wawezeshaji wa wilaya na kata (DFTs na WFTs) jinsi ya kandaa na kusambaza habari zinazohusu sekta ya kilimo kwa njia mbalimbali ili kuiwezesha jamii kupata na kutoa habari katika ngazi ya kijiji, kata, wilaya na kitaifa.

(ii) Wawezeshaji wa wilaya na kata wawezeshe vijiji kwa kushirikisha jamii kuibua mahitaji yao ya habari za kilimo, mifugo, masoko na jinsi watakavyozipata (kwa mfano kupitia redio, luninga, magazeti, mikutano, mabango, ubao wa matangazo, simu n.k.) kwa kuzingatia jinsia na makundi maalumu ambayo ni kama wajane, wazee, vijana, walemavu n.k.

(iii) Halmashauri ziwezeshe jamii na vikundi kuweka utaratibu wa kudadilishana uzoefu (experience sharing) na kupashana habari na kutumia fursa zilizopo (community media, drama and songs) na vituo vya taaluma vya kilimo/mifugo vya kata (WARCs).

(iv) Wanajamii/vikundi wawezeshwe kuweka kumbukumbu za mafanikio, changamoto na matukio (picha) katika kipindi cha utekelezaji wa miradi yao

(v) Halmashauri ianzishe na kuimarisha kitengo cha mawasiliano cha wilaya kwa kujengea uwezo wa upashanaji na utunzaji wa habari *(communication and knowledge management) na kuingiza shughuli zake kwenye mpango.*

9.0 UFUATILIAJI NA TATHMINI YA DADPs

Mwongozo huu unaelekeza mambo yafuatayo kufanyika:

.

i. Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya kilimo ya wilaya ni sharti uwe shirikishi katika hatua zote na ngazi zote kwa kushirikisha wadau wote, na hususan wanufaikaji.

ii. Ni sharti wadau wote pamoja na wanufaikaji washiriki katika kuandaa viashiria vya mafanikio na bao la mantiki (*logical framework*)

iii. Kamati ya mradi itasimamia shughuli za kila siku za mradi

iv. Kamati ya mradi iwasilishe taarifa za maendeleo na shughuli za mradi kwa kamati ya mipango na fedha ya kijiji na kwenye mkutano mkuu wa kijiji kila mwezi na mwisho wa mwaka na pia kwenye mkutano wa ukaguzi wa maendeleo ya mradi na matumizi ya fedha

v. Mkurugenzi wa wilaya aagize taarifa za utekelezaji wa miradi ya jamii/vikundi au wakulima kwa ajili ya majumuisho

vi. Halmashauri iandae utaratibu shirikishi wa kufuatilia maendeleo ya miradi,matumizi ya fedha na matokeo/mabadiliko yanayotokana na utekelezaji wa mradi (kiuchumi, kijamii, kimazingira) (*outcomes)*

vii. Halmashauri iwe na timu inayofuatilia maendeleo ya miradi ya DADPs na kufanya tathmini ya miradi hiyo.Timu hiyo ijengewe uwezo na halmashauri.Timu itawakilisha ripoti zake za ufuatilaji na tathmini kwenye menejiment (CMT)

viii. Halmashauri ziandae taarifa za miradi ya DADPs inayotekelezwa na iliyotekelezwa. Taarifa hizo zionyeshe kama vipaumbele na malengo ya vikundi, vijiji na wilaya yamefanikiwa.Aidha taarifa zionyeshe bayana aina ya ruzuku na matumizi. Kama vile DADG, CBG, EBG na DIDF zikionyesha bajeti, jinsi zilivyoingia na matumizi yake.Halmashauri zitajipima zenyewe kiufanisi kwa kutumia taarifa hizi.

ix. Halmashauri zitanatakiwa kuonyesha fedha zilizobakia na matumizi yake kwenye mwaka mwingine wa fedha (carry over funds)

VIAMBATISHO

Kiambatisho Na.1: Hatua za kuzingatia katika uandaaji wa andiko la mradi

Vipengele vya mradi	Maelezo
Jina la Mradi	Andika jina la mradi (mfano: Ujenzi/ukarabati wa Josho kijiji cha *Magozi*)
Aina ya mradi	Eleza kama mradi ni wa jamii au kikundi
Muda wa mradi	Eleza mradi utatekelezwa kwa muda gani
Muhtasari	Onyesha kwa kifupi vipengele muhimu vya mradi mfano. Kwa nini mradi uwepo, malengo yake, shughuli, matokeo, bajeti n.k
Utangulizi	Toa maelezo mafupi ya jinsi mradi ulivyoibuliwa na utakavyotekelezwa.
Historia fupi ya mradi	Muhtasari wa taarifa na takwimu muhimu kuhusu jamii au kikundi husika Mfano. Ukubwa wa kijiji au kikundi, idadi ya watu, idadi ya wanakikundi, amana walizonazo, mradi iliyopo ya kijiji au kikundi, ufanisi wa miradi iliyotekelezwa hapo nyuma, matumizi ya ardhi ya kilimo, miundombinu, hali ya hewa, uoto wa asili, taasisi zilizopo, changamoto zitakazo tatuliwa kwa uwepo wa mradi, fursa za maendeleo zilizopo n.k
Lengo Kuu	Eleza manufaa ama mabadiliko yatakayopatikana baada ya kutekeleza mradi kwa kipindi cha muda mrefu. Kwa kawaida huchangiwa na miradi mingine katika jamii husika. Lengo kuu linapaswa liendane na malengo ya ASDP.
Lengo Mahsusi	Eleza manufaa ambayo jamii itapata kwa kutekeleza mradi ili kufikia lengo kuu wakati na baada ya utekelezaji. Liwe mahsusi (Specific), lenye kupimika (Measurable), lenye kuweza kufikiwa (Achievable), lenye na uhalisia (Realistic) na lenye ukomo wa muda (Timeframe) yaani "S M A R T"
Matokeo (output/outcome)	Eleza huduma ama bidhaa zitakazozalishwa/zitakazopatikana wakati wa kutekeleza mradi kwa ujumla wake ili kuweza kufikia lengo mahsusi. Mfano: huduma za ugani, miundo mbinu, vifaa, utaalam, uwezo na mavuno.
Shughuli (activities)	Orodhesha kazi zitakazofanyika wakati wa utekelezaji wa mradi ili kuzalisha huduma/bidhaa ambazo kwa ujumla wa shughuli hizo matokeo ya mradi yatafikiwa. Inawezekana kuwa ni kuchimba mtaro, kufyatua tofali, kufundisha n.k.
Nyenzo (inputs	Ainisha mahitaji au vitu ambavyo vinahitajika ili kutekeleza shughuli zilizoorodheshwa na kuleta matokeo yaliyokusudiwa

	katika kufikia lengo mahsusi na hatimaye kuchangia kwenye lengo kuu. Ni muhimu kufahamu kiwango, ubora na idadi au kiasi cha nyezo zinazohitajika. Pia ni lazima kuhakikisha kwamba nyenzo zinatosheleza katika kukamilisha shughuli husika ili mradi usije ukakwama katika utekelezaji. Mfano wa nyenzo ni kama nguvu kazi, vifaa, fedha na rasilimali zingine.
Gharama na manufaa ya mradi	Onyesha mchanganuo wa gharama na manufaa ya mradi (Cost benefit analysis)
Bajeti	Badilisha shughuli zilizo ainishwa kuwa katika mfumo wa fedha yaani kubadilisha kiasi cha mahitaji au nyezo kuwa katika gharama zake. • Ainisha rasilimali au nyenzo zinazohitajika kwa kila shughuli kutoka kwenye taarifa za mbinu shirikishi, jedwali la mikakati ya ufumbizi na shughuli zake, teknolojia mbadala kama vilivyochaguliwa na jamii kwenye kuweka kipaumbele chao. • Ainisha kiasi cha kila rasilimali au nyenzo • Pata bei za kila rasilimali au nyenzo • Kokotoa au tafuta jumla ya gharama • Onyesha mgawanyo wa gharama kwa kila mchangiaji/mdau.
Ugharamiaji	Onyesha mgawanyo wa gharama kwa kila mchangiaji/mdau.
Uendeshaji na utekelezaji	Eleza ni kwa namna gani mradi utatekelezwa na kusimamiwa kwa kuonyesha majukumu ya kila muhusika. Mfano majukumu ya kamati ya mradi, Wafaidikaji, Serikali ya kijiji. Andaa mpango wa utekelezaji Eleza jinsi Ufuatiliaji na Tathmini utakavyofanyika.
Masoko	Eleza upatikanaji wa masoko pamoja na kiwango cha ushindani kilichopo.
Manufaa/Matokeo ya muda mrefu	Eleza ongezeko la kipato, manufaa yatakayopatika kiuchumi na kijamii.
Masuala Mtambuka (Hifadhi ya Mazingira, VVU/UKIMWI, Jinsia)	Eleza ni kwa jinsi gani utazuia matokeo yasiyotarajiwa ya utunzaji wa mazingira (ESMF), Elezea jinsi mnavyo kabiliana na masuala ya VVU/UKIMWI na jinsia.
Uendelevu wa mradi (sustainability)	Eleza ni kwa jinsi gani jamii itashiriki kuhakikisha uendelevu wa shughuli za mradi.
Dhanio la Mradi (Project risks and Assumptions)	Elezea mambo halisi yaliyo nje ya uwezo wa mradi lakini ni muhimu kuwepo au kutokea ili mradi ufanikiwe

Kiambatisho Na. 2: Bao Mantiki (Logical Framework)

Ni zana inayoweka kwa muhtasari mtiririko wa kimantiki wa mradi ulivyotayarishwa. **Yaani** mahitaji au nyenzo na rasilimali zote zinazohitajika zinapatikana ndipo shughuli zilizopangwa zitafanyika, na ndipo matokeo yatarajiwayo yataonekana, hivyo malengo mahsusi yaliyopangwa yatafikiwa na ndipo lengo kuu litafikiwa. Hivyo kila andiko litakalogharamiwa na DADP lazima liwe na bao la mantiki ili kubaini mantiki ya mradi na kurahisisha ufuatiliaji na tathmini.

(i) Muundo wa Bao Mantiki

- Lina mihimili minne na safu nne
- Mhimili wa kwanza kushoto huitwa muhtasari, wa pili viashiria, wa tatu vyanzo vya uhakiki na wa nne mambo yafikiriwayo au yatarajiwayo.
- Safu ya kwanza huitwa safu la lengo kuu la maendeleo (shaba ha kuu) safu hii hueleza taarifa zote zinazohusu lengo kuu.
- Safu ya pili huitwa safu ya malengo mahsusi na hueleza taarifa za malengo mahsusi
- Safu ya tatu huitwa safu ya matokeo. Hueleza taarifa zote za matokeo yote ya mradi vikiwemo viashiria na vyanzo vya taarifa za uhakiki
- Safu ya nne huitwa safu ya shughuli. Huelezea shughuli zote kwa kila tokeo la mradi. Pia huelezea nyenzo zote na rasilimali kwa kila shughuli. Huonyesha viashiria vya shughuli

(ii) Hatua za Kuunda Bao Mantiki (Hatua)

- Andaa uchambuzi wa mikakati au ufumbuzi wa tatizo kikamilifu kwa kutumia mti wa matatizo na mti wa matumaini.
- Hamishia taarifa zilizo katika jedwali la ufumbuzi wa tatizo na matokeo yake, shughuli zake, maelezo yake ziandike kwenye jedwali la Bao Mantiki ukijaza mhimili wa kwanza toka juu hadi chini.
- Endelea kujaza mhimili wa pili na wa tatu hadi wa nne ukianzia chini, yaani mhimili wa kwanza safu ya nne inayoelezea shughuli, tazama *Jedwali* hapo chini.

MUUNDO WA BAO MANTIKI

Muhtasari	**Viashiria**	**Vyanzo vya uhakiki wa viashiria**	**Mambo ya kufikirika au yatarajiwayo**
HATUA YA KWANZA **<u>Lengo kuu</u>** Uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara umeongezeka	***HATUA YA TATU*** • Ongezeko la uzalishaji kwa eneo • Asilimia ya kaya zilioongeza kiwango cha uzalishaji wa mazao kwa eneo.	***HATUA YA NNE*** Taarifa kutoka afisa kilimo , kamati ya mradi na serikali ya kijiji	***HATUA YA PILI***
<u>Lengo Mahsusi</u> Kaya zinazotumia kilimo cha umwagiliaji zimeongezeka kutoka **x** mwaka **xx** kufikia **y** mwaka **yy**	Idadi ya kaya zinazotumia kilimo cha umwagiliaji	Taarifa kutoka afisa kilimo , kamati ya mradi na serikali ya kijiji	Kaya kutumia pembejeo, teknolojia bora za uzalishaji na Vyanzo vya maji kuhifadhiwa
<u>Matokeo</u> i. Miundo mbinu ya umwagiliaji ya asili iliyoboreshwa. ii. Uzalishaji umeongezeka kutoka tani **x** mwaka **xx** kufikia tani **y** mwaka **yy** kwa ekari.	• kuwepo kwa banio na mfereji mita xx ulioboreshwa • tani za zao zilizoongezeka • Ongozeko la mazao yanayolimwa kwa msimu	Taarifa kutoka kamati za mradi.	Kupatikana kwa pembejeo na teknolojia bora za uzalishaji
<u>Shughuli</u> Ujenzi wa banio la maji Ujenzi wa Mfereji mkuu mita **x** Mafunzo **(taja aina ya mafunzo)** kwa wakulima **xx**	<u>Shabaha</u> • Uwepo wa mkandarasi • Kiasi cha mchango wa jamii • Idadi ya wakulima waliopata mafunzo(taja) katika muda muafaka	• Taarifa kutoka kamati za mradi. • Mikataba na mkandarasi • Taarifa ya ujenzi ya mkandarasi na wasimamzi • Taarifa za mafunzo	Kupatikana kwa fedha na Mkandarasi kwa wakati muafaka

Nyenzo Aina na gharama zinazohitajika - gharama za mkandarasi - gharama za mafunzo - gharama za usimamizi	kiasi cha fedha kilichotumika kwa ujenzi na mafunzo.	Mifumo ya udhibiti Taarifa za fedha na manunuzi	

Kiambatisho Na.3: Utaratibu wa uchangiaji katika kutekeleza miradi mbalimbali ya uwekezaji katika jamii/vikundi

Eneo la uwekezaji	**Ruzuku (serikali)**	**Wanufaikaji**
Mazingira	95%	5%
Miundombinu ya uzalishaji na masoko	80%	20%
Miradi ya vikundi ya uzalishaji mazao kwa kutumia pembejeo na ununuzi wa madawa ya mifugo	50%	50%
Uwezekaji kwenye vikundi kwa ajili ya kuendeleza teknolojia	80%	20%
Miradi ya ufugaji (kununua mifugo bora)	80%	20%
Uwekezaji katika kilimo kupitia vikundi au jamii	80%	20%
Uwekezaji katika kuongeza thamani (agro-processing) k.m. mashine za kusindika n.k.	80%	20%

Kiambatisho Na. 4: Vigezo vinavyotumika kuhakiki mradi

Kipengele	**Maelezo**
1. Walengwa	- Nani anayenufaika na mradi - Nani mlengwa - Mradi unalenga/unakidhi mahitaji ya walengwa? - Je kuna watu wengine watakaonufaika na huo mradi?
2. Ushirikishwaji	- Je jamii ipo tayari kuchangia? - Jamii inachangia kwa njia gani?
3. Masuala ya kitaalam	- Timu ya watekelezaji imejipangaje/vipi - Wana utaalamu/stadi wote - Utaalam/stadi wa ziada utapatikana wapi?
4. Gharama	- Vifaa na nguvu kazi vinaonyeshwa kwenye andiko la mradi?

	bajeti yake ipo na ni halisia?
5. Masoko	- Soko kwa ajili ya mazao lipo? - Ushindani wa bei upo? - Ipi Mikakati mingine - Wakati na kipindi cha soko
6. Athari	- Zitakazotokana na tekinolojia zitakazotumiwa - Mbinu za kupunguza/kukabiliana na athari hizo
7. Jinsia na masuala mengine mtambuka	- Wamiliki – ni nani (Me, Ke, Vijana) - Watakaonufaika(Me, Ke, Vijana) - Makundi mbalimbali yameshirikishwa - Je masuala ya mazingira,usalama wa chakula,matumizi ya ardhi na upashanaji habari yamezingatiwa?
8. Mpangilio/utaratibu wa utekelezaji	- Mradi utaanza lini na kumalizika lini - Utaratibu wa kupata washauri waelekezi - Nani anayehusika
9. Taasisi nyingine	- Kufahamu taasisi au asasi zenye mwelekeo sawa na ASDP - Jinsi ya kuboresha mahusiano/mashirikiano
10. Uendelevu	- Jamii imejiwekea mikakati ya kuendeleza mradi baada ya kumalizika/kukoma ufadhili? - Kushauri maeneo au mikakati ya endelevu kama haipo.
11. Manufaa ya mradi	- Je kumefanyika mchanganuo wa kubaini gharama na manufaa ya mradi kiuchumi, kijamii na kifedha?
12. Tathmini na Ufuatiliaji	- Andiko linaonyesha jinsi ya ufuatiliaji na tathmini vitafanyika vipi?

Kiambatisho Na 5: Jinsi ya kuchanganua Gharama na Manufaa (Cost-Benefit Analysis) ya Mradi

Kuchanganua au kupembua gharama na manufaa ya mradi ni mchakato wa kufahamu na kulinganisha gharama na manufaa ya mradi. Mradi wenye tija ni ule ambao manufaa yake yanazidi gharama za uwekezaji na uendeshaji na yanaweza kuwa ya kifedha, kiuchumi na ya kijamii.

5.1 Hatua za Kuchanganua Gharama na Manufaa

i. Ainisha gharama za mradi kama ifuatavyo:

Gharama za mradi zimegawanyika katika maeneo ya uwekezaji na uendeshaji kama ifuatavyo:

Gharama za uwekezaji:

- Gharama za kuendeleza ardhi (*land development costs*) kama kukodi au kununua ardhi
- Gharama ya nyenzo au bidhaa (costs of *physical goods*) kama mbolea, viuatilifu, vifaa vya ujenzi n.k

Gharama za uendeshaji

- Gharama za nguvu kazi (*labour costs*) kama vibarua, wataalam na wanafamilia
- Gharama za kodi na ushuru (*taxes*)
- Ada za benki na vyombo vya fedha (*Bank charges*)
- Tahadhari (*Contingencies*) kama mfumuko wa bei

:

ii. Ainisha manufaa ya mradi kama ifuatavyo.

Manufaa ya mradi yanaweza kuwa ongezeko la uzalishaji na tija ya mazao ya kilimo na mifugo, ongezeko la kipato, ubora wa bidhaa, kupatikana kwa fursa za ajira n.k.

5.2 Namna ya Kukokotoa Manufaa ya Kifedha

Ili kufahamu iwapo mradi uliondaliwa una manufaa au hapana inapaswa Wafaidika na DFT kuchanganua mambo yafuatayo: (i) Mapato ghafi (Gross revenue); (ii) Faida ghafi (Gross Profit); (iii) Faida halisi (Net profit); na (iv) Kipindi cha kurejesha gharama za uwekezaji (**Pay back- Period**).

1) Mapato ghafi (Gross Revenue)

Mapato ghafi hupatikana kwa **kuzidisha** ongezeko la uzalishaji **na** bei ya zao/bidhaa **kisha toa** gharama za uzalishaji za mzunguko mmoja tu wa uzalishaji.

Mfano: Kilimo cha umwagiliaji; mfereji umeboreshwa kwa gharama za DADG Sh 30,000,000 na kuongeza mavuno ya mpunga katika kijiji cha Kibaoni toka kilo 1,000 ,000 mwaka 2005 kufikia kilo 1,500,000 mwaka 2006.

Taarifa: 1. Bei ya mpunga: Shs. 5,000 kwa gunia la kilo 80

2. Gharama za uzalishaji

- Mbegu	500,000
- Kuandaa hadi kulima	6,000,000
- Kuamia ndege (bird scaring)	500,000
- Kuvuna	1,000,000
- Kupura	1,000,000

JUMLA
9,000,000

(Tambua gharama za uzalishaji za mzunguko mmoja wa uzalishaji (Direct Variable costs)

Mapato ghafi = [(1,500,000 – 1,000,000) x 5,000] - 9,000,000
80
= (500,000 x 5,000) – 9,0000,000
80
= 22, 250,000

Angalizo:

1. Gharama za zana za uzalishaji zinazotumika zaidi ya mzunguko mmoja wa uzalishaji au msimu mmoja hazitumiki kukokotoa mapato ghafi kwa vile zitaendelea kuleta manufaa kwa zaidi ya mzunguko mmoja wa uzalishaji au msimu
2. Gharama zinginezo ambazo hazihusiki na uzalishaji moja kwa moja hazitumiki katika kukokotoa mapato ghafi (k.m Usimamizi, magunia, usafirishaji toka shambani /nyumbani hadi sokoni, madawa ghalani,utunzaji na ulinzi ghalani, riba, uchakavu, kodi na ushuru)
3. Gharama za uzalishaiji ndizo anazolipa mkulima/mlengwa na zinatumika katika kuzalisha tu; kwa sababu hiyo haya ndiyo manufaa yaliyo muhimu zaidi kwa mkulima na ndiyo yanayofaa kuzingatiwa kwani ndiyo muhimu kwa kuendesha mradi na uendelevu wake. Gharama za kuwekeza/kutekeleza mradi haziendeshi mradi wala manufaa mengineyo yasiyo ya moja kwa moja wala yasiyo ya kifedha hayatumiki kuendesha mradi
4. Pia zingatia manufaa mengine yasiyo ya moja kwa moja kama yapo

2) Faida ghafi (Gross Profit)

Hupatikana kwa kutoa Gharama zingine za uendeshaji(operating cost) **kwenye mapato ghafi isipokuwa gharama** za uchakavu wa zana, riba na kodi/ushuru. **.**

Mfano:

TAARIFA/TAKWIMU

1. Mapato ghafi ni **11,250,000**
4. Gharama zingine za uendeshaji

- Ukarabati (maintenance)	300,000
- Ununuzi (maguni n.k.)	100,000
- Usimamizi	50,000
- Usafirishaji	350,000
- Ulinzi	50,000

- Madawa ghalani	100,000
- Utunzaji gharani	50,000
JUMLA	**1,000,000**

Faida ghafi = 22, 250,000 – 1,000,000
= 21,250,000

Angalizo:

1. Gharama za zana za uzalishaji zinazotumika zaidi ya mzunguko mmoja wa uzalishaji au msimu mmoja hazitumiki kukokotoa faida ghafi
2. Gharama za uchakavu wa zana, riba na kodi hazitumiki katika kukokotoa faida ghafi

Manufaa haya yanafaa zaidi kwa sekta binafsi itakayoshiriki katika kufanikisha miradi ya vikundi au jamii kwa kuuza bidhaa zake au huduma zake.

3) Faida halisi (Net profit)

Hupatikana kwa ku**toa** gharama **nyinginezo kama** za uchakavu wa zana, riba na kodi/ushuru kwenye faida ghafi

Mfano:

TAARIFA

1. Faida Ghafi shilingi **21,250,000**

2- Uchakavu	25,000
- Ushuru/kodi	10,000
- Riba	100,000
JUMLA	**135,000**

Faida Halisi = 21,250,000– 135,000
= 21,115,000

Angalizo:

- Gharama zote zinatumika kukokotoa Faida halisi
- Gharama za zana za uzalishaji zinazotumika msimu mmoja hazitumiki kukokotoa faida ghafi.
- Gharama za uchakavu wa zana, riba na kodi hazitumiki katika kukokotoa faida ghafi ila faida halisi
- Manufaa haya yanafaa zaidi kwa sekta binafsi itakayoshiriki katika kufanikisha miradi ya vikundi au jamii kwa kuuza bidhaa au huduma zake

4) Kipindi cha kurejesha gharama za uwekezaji (Pay-Back Period)

1. Tambua chanzo cha manufaa na zao/bidhaa/huduma
2. Kokotoa kiasi cha zao/bidhaa za huduma hiyo
3. Tambua bei ya zao/bidhaa/huduma hiyo katika soko

4. Tambua gharama za uwekezaji au kutekeleza mradi
5. Kokotoa Kipindi cha kurejesha gharama za uwekezaji kwa **kujumulisha** ongezeko la manufaa/mapato kwenye kipindi chote cha utekelezaji mradi (Misimu miwili/mizunguko miwili ya uzalishaiji **gawia/gawanya** kwa gharama za uwekezaji/ kutekeleza mradi hadi upate tarakimu iliyo zaidi ya sufuri.
6. Mradi unaoonyesha gharama hasi kwa mda zaidi ya mwaka mmoja sio muafaka.

Mfano wa kukokotoa kipidi cha kurudisha gharama

Mtiririko wa Fedha	Mwaka 1	Mwaka 2	Mwaka 3	Mwaka 4	Mwaka 5
Mapato ghafi yanayotarajiwa ('000 Tsh)	22,250	40,000	40,000	40,000	40,000
Gharama za uwekezaji ('000 Tsh)	30,000	0	0	0	0
Gharama za uzalishaji ('000 Tsh)	10,000	10,000	10,000	10,000	10,000
Gharama zinginezo ('000 Tsh)	135	135	135	135	135
Mapato Halisi ya Mradi	0	29,865	29,865	29,865	29,865
Mkusanyiko wa Manufaa	-17,885	11,980	41, 845	71,710	101,575
Kipindi cha Kurudisha Gharama	Kipindi cha kurudisha gharama ni Mwaka 3				

Kiambatisho Na 6: DADP STRUCTURE

1. Executive Summary.

- Write in summary the process involved in the preparation of DADP (village phasing out process, participatory planning (Extended O&OD)
- Mention major identified agriculture and livestock problems
- Mention proposed solutions/interventions by farmers
- Mention projects identified to combat the problems
- Mention district priorities
- Mention total financial resources required to finance the DADP and categorically identify types of sources.
- Finalize the section by mentioning key targets expected to be achieved in three years.

2. District profile

a. Location
b. Administration
c. Climate
d. Physical features (Agriculture land, Vegetation, rivers etc)
e. Infrastructure (Roads, railway, communication, power supply)
f. Agriculture potentials (Types and status of Crops and livestock kept)
g. Supporting institutions

3. District Agriculture situation analysis/SWOT

4. Policy and Strategies:

a. Agriculture/ livestock, Cooperative, microfinance , Fisheries policy
b. Agricultural Sector Strategy (ASDS)
c. ASDP- (DADPs)

5. Vision statement of the council

6. Mission statement of the council

7. Objective and targets

8. Review of previous DADP (2006/07, 07/08 ,2008/09) and mid- year report FY 2009/10

a. Summarize the physical and financial performance focusing on key output and outcomes for previous years and on performance by activity for the mid-year report :

Planned target	**Planned activities**	**Approved budget**	**Amount received**	**Expenditure**	**Physical achievement** (***output & outcome)***	**Remarks**

b. Way forward

i. Summarize key problems in the implementation of DADP.
ii. Summarize strategies set to improve the implementation performance
iii. Provide the summary of pending activities expected to be implemented from January to June

9. Summary of Investment Projects planned for year 2010/11

Projects/ Interventions	**Place/ villages**	**Planned Budget**	**Sources of funds**					
			DADG* (Tshs)	**CBG**	**EBG**	**ongoing projects**	**Council contribution**	**Community contribution**

* ***Write –ups for Investment project indicated in this table should be attached as appendix 1***

10. **District proposed Priority Agriculture interventions.(planrep)**
11. **Action plan.**
12. **Procurement plan**.
13. **M and E Plan**

APPINDIX 1: DADPs Project Write -ups